



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CDC/A.10/17/VOL III/5

09 Machi, 2023

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kufuatia kutolewa kwa kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/360/01"A"/48 cha tarehe 26 Januari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Chamwino anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 2**

**SIFA:** Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne / cha sita waliohitimu mafunzo ngazi ya Astashahada/Cheti NTA Level 5 katika mojawapo ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii, Mipango na Sayansi ya Siasa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chou chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**MAJUKUMU**

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- IV. Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halamshauri ya Kijiji
- V. Kutafsiri na kusimamia sera Sheria na Taratibu
- VI. Kuandaa taarifa za Utekelezaji na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji.
- VIII. Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za vijiji.

## NGAZI YA MSHAHARA.

Mshahara ni kwa Mujibu wa viwango vya mishahara Serikalini yaani TGS B kwa mwezi.

## MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.
2. Mwombaji awe na umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed C.V)
4. Maombi yote waombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. Testimonials "provisional results" "statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULT SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
9. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **22/03/2023** saa **9:30** alasiri
10. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino,  
S.L.P 1126,  
**CHAMWINO- DODOMA**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino [www.chamwinodc.go.tz](http://www.chamwinodc.go.tz)



Dkt. Semistatus H. Mashimba

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**

HALMASHAURI  
MKURUGENZI MTENDAJI  
S. L. P. 1126  
DODOMA